USHIRIKA MUTAKATIFU

yaani CHAKULA CHA BWANA

MAFUNDISHO

Yesu aliagiza wanafunzi wake kumukumbuka kwa njia ya mukate na mvinyo. Tangu mwanzo wa kanisa, wakristo wametii agizo lake, wakikumbuka maisha yake ya kutii Mungu Baba, na kifo chake cha kuokoa wenye zambi.

Ushirika Mutakatifu una maana nyingi. Wakati tunajitayarisha mbele ya ibada, na wakati tunafika karibu na meza takatifu, ni vema kuwaza juu ya moja au mawili ya maneno haya:

- Yesu alitoa mwili wake musalabani kutuokoa: tutubu makosa yetu.
- Tukumbuke tena zawadi ya uzima wa milele, na kulishwa kiroho na Yesu mwenyewe.
- Tushukuru Mungu kwa mapendo yake makubwa kwetu.[1]
- Nyuma ya kukaa mezani na wanafunzi, Yesu alikwenda kufanya mapenzi ya Baba yake. Sisi vile tutoke kwa Ushirika na nia tayari kutii Mungu na kufanya kazi yake duniani.[2]
- Usiku ule, Yesu aliahidi wanafunzi wake kwamba Roho Mutakatifu atawaletea faraja, shauri na nguvu. Wakati wa Ushirika, tuombe Mungu kutimiza ahadi hii.
- Yesu aliomba Mungu kupatia wafuasi wake umoja. Tukumbuke umoja wetu pamoja na wakristo po pote duniani, na zaidi umoja wetu na wanaopokea mukate na mvinyo pamoja nasi.

Katika miaka mingi ya hadizi ya kanisa, wakristo wamefundisha mambo mbalimbali juu ya Ushirika Mutakatifu. Wengine wamesema kwamba mukate na mvinyo zinageuka ndani yao, kuwa mwili na damu za Yesu, kwani Yesu alisema kwa wanafunzi wake, "Huu ni mwili wangu, hii ni damu yangu". Lakini inaonekana kwamba Yesu alitaka kuwaelezea kweli ya kiroho, sawasawa alivyojitaja nuru ya dunia, muchungaji, na muzabibu. Kwa hivi, katika ibada hii, tunapokea mukate na mvinyo kwa kimwili; lakini kwa kiroho, kwa njia ya imani yetu na musaada wa Roho Mutakatifu, tunazidisha ndani yetu uzima wa Yesu aliyekufa kwa ajili yetu.

Ibada hii ina sehemu mbalimbali:

Kukutana mbele ya Mungu
Kupokea Neno la Mungu
Maombi ya watu wa Mungu
Salama ya Bwana
Chakula cha Bwana
Kutoka kwa watu wa Mungu

MAAGIZO

A KUJITAYARISHA. Kila mutu anayekuja kupokea sakramento ya Ushirika Mutakatifu ajitayarishe nyumbani kwa kujitambua, kuomba na kusoma Biblia.

B KASISI MWONGOZI WA IBADA. Ni lazima kwamba kasisi mwenye kuongoza ibada ya Ushirika awe kasisi aliyeamuriwa na Askofu wa Kanisa la Ushirika Anglikana. Wakati Askofu ya Dayosisi yuko, yeye awe kasisi mwongozi wa ibada, lakini anaweza kusaidiwa na kasisi mwingine, au anaweza kuruhusu kasisi mwingine kuongoza.

Kasisi mwongozi anakaribisha watu; anasema ondoleo la zambi, sala ya siku, salama, na baraka; anasema Ombi la Kushukuru na kuvunja mukate.

Kasisi mwongozi anaongoza ibada kufuatana na maagizo hapa chini, na matayarisho anayofanya mbele ya wakati, na uongozi wa Roho Mutakatifu.

C Ni vema kusema AMRI KUMI zote wakati wa KUJA na wakati wa KUFUNGA. Amri Kumi zinaweza kusemwa vilevile namna zimeandikwa kwa ukurasa 76.

D MATANGAZO yanaweza kutangazwa nyuma ya kipande kisicho Habari Njema, mbele ya Maombi ya Kanisa, au nyuma ya baraka.

E Kama DIKONI yuko, anasoma Habari Njema, akasaidia Kasisi na kazi nyingine.

F OMBI LA KUSHUKURU. Kasisi mwongozi atachagua moja la maombi yale matatu: 22a, 22b, au 22c. Ndani yake afanye matendo fulani, pa kila alama:

(a) Atwae sahani mikononi mwake.
(b) Avunje mukate.
(c) Aweke mukono wake juu ya mukate wote.
(d) Atwae kikombe mikononi mwake.
(e) Aweke mukono wake juu ya kila kikombe au chupa cha mvinyo.

G Ombi la Kushukuru (22a au 22b au 22c) ni ombi moja: inafaa au kusimama au kupiga magoti toka mwanza hata mwisho. Kasisi aeleze kwa watu wafanye nini mbele ya kuanza Ombi hili.

H Afazali mukate na mvinyo zinatumiwa, lakini kama mukate au mvinyo haipatikani, kitu kingine kinaweza kutumiwa, kinachokubaliwa na Dayosisi.

I Wakati wa kutayarisha meza ni vema kama kasisi ananawa mikono.

J Wenye kugawa mukate na mvinyo kwa watu ni wakasisi, wadikoni na wengine waliokubaliwa na Askofu wa Dayosisi.

USHIRIKA MUTAKATIFU

yaani CHAKULA CHA BWANA

1 *Wakati wahudumu wanapoingia watu waimbe zaburi au wimbo.*

2† *Shairi la siku lisomwe.*

3 *Kasisi akaribishe watu na maneno haya:*
Bwana awe nanyi
Wote **Awe pia nawe.**
Kutoka Ufufuko hadi Pentekote, Kasisi aseme:
Aleluya! Kristo amefufuka.
Wote **Amefufuka kweli. Aleluya!**

4† *Wote wapige magoti na waseme moja la maombi haya:*

— — — — □ — — — —

4a† **Mungu Mwenyezi,**
kwa hivyo kwako mioyo yote ni wazi,
mahitaji yote yamejulikana,
wala hakuna siri lililofichwa;
uyasafishe mawazo ya mioyo yetu
kwa kuingiza Roho yako Mutakatifu,
ili tukupende kwa ukamilifu
na kulitukuza Jina lako takatifu,
kama inavyotustahili;
kwa Kristo Bwana wetu. Amina

- - - - - - - - - - - - *AU*- - - - - - - - - - - -

4b† **Mwenyezi Mungu,**
unatia kwa nuru yaliyofichwa gizani,
unajua vivuli vya mioyo yetu:
kwa Roho yako utusafishe,
utuamushe, utufanye wapya,
ili tutembee kwa nuru,
na tutukuze jina lako,
kwa Yesu Kristo, Nuru ya dunia. Amina.

— — — — — — — — — — □ — — — — — — — — — —

5† *AMRI KUMI au AMRI MBILI za Bwana wetu zisomwe na muhudumu akisimama, watu wakipiga magoti.*

— — — — □ — — — —

5a† AMRI KUMI

Bwana wetu Yesu Kristo alisema, kama mukinipenda mutatii amri zangu; afazali heri wale wenye kusikia Neno la Mungu na kulishika. Sikieni amri hizi Mungu alizoziagiza watu wake, na muziweke rohoni.

1. Mimi ni Bwana Mungu wako, usiwe na miungu mingine ila mimi. Upende Bwana Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili yako yote, na kwa nguvu yako yote.

Jibu **Bwana, uturehemu, utuelekeze mioyo yetu tuishike amri hii.**

2. Usijifanyie sanamu. Mungu ni roho, nao wenye kumwabudu, sharti wamwabudu katika roho na kweli.

3. Usilitaje jina la Bwana Mungu wako bule, lakini utolee Mungu kumwabudu kumupendeza, pamoja na heshima na woga.

4. Kumbuka siku ya Mungu uitakase. Kristo amefufuka, tia mafikili yako juu ya maneno ya juu, wala si juu ya maneno yaliyo duniani.

5. Heshimu baba yako na mama yako, uishi kama mutumishi wa Mungu, uheshimu watu wote, upende ndugu zako.

6. Usiue, jua lisishuke na uchungu wako haujakwisha bado, ushinde ubaya kwa mema.

7. Usizini, ujue mwili wako ni hekalu la Roho Mutakatifu aliye ndani yako.

8. Usiibe, lakini zaidi utumike, ufanye kazi njema kwa mikono yako, uwe na kitu cha kugawia mwenye kuhitaji.

9. Usimushuhudie jirani yako uwongo, lakini useme kweli katika mapendo.

10. Usitamani chochote kilicho cha jirani yako. Kumbuka maneno ya Bwana Yesu, kama alivyosema: Upende jirani yako kama wewe mwenyewe, Basi, mapendo ni utimilifu wa sheria.

Jibu **Bwana, uturehemu, tunakusihi uziandike amri zako hizi zote, mioyoni mwetu.**

- - - - - - - - - - - - *AU* - - - - - - - - - - - -

5b† AMRI MBILI ZA BWANA WETU

Bwana wetu Yesu Kristo alisema: Bwana Mungu wetu ni Bwana mumoja, na upende Bwana Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili yako yote, na kwa nguvu yako yote. Amri ya kwanza ndiyo hii.

Ya pili ndiyo hii; Upende jirani yako kama wewe mwenyewe. Hii ndiyo amri mupya ninawapa ninyi, mupendane; kama mimi nilivyowapenda ninyi.

Jibu **Bwana uturehemu, tunakusihi uziandike Amri zako hizi zote mioyoni mwetu.**

— — — — — — — — — — — — — — — — — — — —

6 *Kasisi asome mbili au zaidi ya mashairi haya.*

Sikieni maneno ya kutia moyo yaliyosemwa na Mwokozi wetu Yesu Kristo kwa wote wanaomukujia kwa kweli: Kujeni kwangu, ninyi wote munaosumbuka na wenye muzigo muzito, nami nitawapumzisha ninyi. *Matayo 11:28*

Sikieni maneno ya Paulo Mutakatifu:

Neno hili ni aminifu, na linastahili kukubaliwa na watu wote, ya kwamba Kristo Yesu alikuja kwa dunia kuokoa wenye zambi. *1 Timoteo 1:15*

Sikieni maneno ya Yoane Mutakatifu:

Na kama mutu akitenda zambi, tuna Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki, naye ni kipatanisho kwa zambi zetu. *1 Yoane 2:1-2*

Kwa maana Mungu alivyopenda ulimwengu, hata kutoa Mwana wake wa pekee, ili kila mutu akimwamini asipotee, lakini apate uzima wa milele. *Yoane 3:16*

7 *Halafu Kasisi aseme:*
Tunyamaze kidogo kukumbuka zambi zetu.

Halafu aseme:
Tukiri zambi zetu na kutubu na imani; tukikusudia kushika amri za Mungu na kukaa katika mapendo na salama na watu wote.

Wote: **Mungu Mwenyezi,**
Baba yetu ya mbinguni,
tumekosea wewe,
na tumekosea jirani zetu
kwa mawazo yetu,
na kwa maneno yetu,
na kwa matendo yetu,
na kwa maovu tuliyoyatenda,
na kwa mema tusiyoyatenda,
kosa letu wenyewe.
Sisi tunatubu kabisa.
Kwa ajili ya Bwana wetu Yesu Kristo,
utusamehe yote yaliyopita;
utuwezeshe tangu leo kukutumikia,
katika upya wa uzima,
kwa utukufu wa Jina lako. Amina.

8 *Kasisi atangaze kuondolewa kwa zambi.*

Mungu Mwenyezi, mwenye kusamehe wote wanaotubu kwa kweli; a*wa*rehemu, a*wa*samehe, a*wa*okoe kwa zambi ze*nu* zote, a*wa*sibitishe,‡ a*wa*pe nguvu kwa wema wote, na a*wa*linde katika uzima wa milele; kwa Yesu Kristo Bwana wetu. **Amina.**

9† *UTUKUFU usemwe au uimbwe (ona ukurasa 22).*
Utukufu kwa Mungu, juu mbinguni,
na salama duniani,
kwa watu wanaomupendeza,
tunakusifu, tunakubariki,
tunakuabudu, tunakutukuza,
tunakushukuru kwa ajili ya utukufu wako mukuu.
Bwana Mungu, Mufalme wa mbinguni,
Mungu Baba Mwenyezi,
Ee Bwana, Mwana pekee Yesu Kristo;
Ee Bwana Mungu, Mwana kondoo wa Mungu,
Mwana wa Baba, unayeondoa zambi za dunia, Uturehemu.
Unayeondoa zambi za dunia, upokee ombi letu.
Unayekaa kuume kwa Mungu Baba, Uturehemu.
Kwa maana wewe peke yako Mutakatifu,
wewe peke yako Bwana,
wewe peke yako, Ee Kristo,
pamoja na Roho Mutakatifu,
uliye juu kwa utukufu wa Mungu Baba. Amina.

KUPOKEA NENO LA MUNGU

10 *Kasisi aseme SALA YA SIKU, akianza hivi:*
Bwana awe nanyi
Wote **Awe pia nawe.**
Kasisi Tuombe...

11 *Masomo mawili au matatu kutoka Maandiko Matakatifu yasomwe, la mwisho liwe la Habari Njema.*

12 *Kuketi. Kipande kinachotoka katika AGANO LA KALE kisomwe. Musomaji aseme kwanza:*

Sikieni Neno la Bwana
kama lilivyoandikwa katika ...

Na kwa mwisho aseme: Hilo ndilo Neno la Bwana.
Wote **Asante kwa Mungu.**

13* *Zaburi au wimbo unaweza kusomwa au kuimbwa.*

14 *Kuketi. Kipande kinachotoka katika AGANO JIPYA kisomwe. Musomaji aseme kwanza:*
Sikieni Neno la Bwana
kama lilivyoandikwa katika ...

Na kwa mwisho aseme: Hilo ndilo Neno la Bwana.
Wote **Asante kwa Mungu.**

15* *Zaburi au wimbo unaweza kusomwa au kuimbwa.*

16 *Kusimama. Kipande cha HABARI NJEMA kisomwe. Musomaji aseme kwanza:*
Sikieni Habari Njema takatifu,
kama ilivyoandikwa katika ...
Wote **Utukufu uwe nawe, Ee Bwana wetu.**

Mwisho wa kusoma Habari Njema, musomaji aseme:
Hii ndiyo Habari Njema ya Kristo.
Wote **Tunakusifu sana, Ee Kristo,**
kwa Habari Njema yako takatifu.

17 *KUHUBIRI*
Mahubiri yanaweza kujibiwa na maombi mafupi, wimbo, au kunyamaza.

18† *Kusimama. IMANI YA NIKE*
Ninamwamini Mungu mumoja, Baba Mwenyezi,
Muumba wa mbingu na dunia,
na vitu vyote vinavyoonekana na visivyoonekana.

Ninamwamini Bwana mumoja, Yesu Kristo,
Mwana wa pekee wa Mungu,
amezaliwa na Baba mbele ya kuwa ulimwengu,
Mungu kutoka Mungu, Nuru kwa Nuru,
Mungu kweli kwa Mungu kweli,
amezaliwa, hakuumbwa,
Mwenye umungu mumoja na Baba.
Vitu vyote viliumbwa naye.
Alishuka toka mbinguni,
kwa ajili ya sisi watu,
na kwa ajili ya wokovu wetu;
alitwaa mwili kwa tendo la Roho Mutakatifu,
katika Bikira Maria,
akawa mutu.
Akasulibiwa kwa ajili yetu,
wakati wa Pontio Pilato,
akateswa, akazikwa,
Akafufuka kisha siku tatu,
kama ilivyoandikwa;
akapanda mbinguni,
anakaa kwa mukono wa kuume kwa Baba.
Ndipo atarudi kwa utukufu,
kuwahukumu wazima na wafu,
na ufalme wake hautakuwa na mwisho.

Ninamwamini Roho Mutakatifu,
Bwana na Mutoa uzima,
aliyetoka kwa Baba na Mwana,
anayeabudiwa na kutukuzwa,
pamoja na Baba na Mwana,
aliyesema kwa manabii.

Ninaamini Kanisa, moja, takatifu, katolika,‡
lililotoka kwa Mitume.
Ninasadikia ubatizo mumoja
kwa kuondolewa kwa zambi.
Ninangojea ufufuko wa wafu
na uzima wa milele utakaokuja. Amina.

MAOMBI YA KANISA

19† *Muhudumu atumie au 19a, au 19b au 19c.*

— — — — Ú — — — —

19a *Muhudumu* Tuombee Kanisa na dunia na tumushukuru Mungu kwa wema wake wote.

Tukumbuke waaskofu wote, na hasa Askofu Mukuu yetu J, na Askofu ya Dayosisi yetu J, na waongozi wengine wa makanisa yote: wawe na hekima na umoja.

Wote **Bwana mwema utusikie.**
Muhudumu Wakubwa wa inchi yetu watawale na haki.
Wote **Bwana mwema utusikie.**
Muhudumu Haki iwe ngabo na mulinzi wetu.
Wote **Bwana mwema utusikie.**
Muhudumu Inchi iwe salama; na watu wabarikiwe.
Wote **Bwana mwema utusikie.**
Muhudumu Makundi ya wanyama yaongezeke; na samaki baharini ziwe nyingi.
Wote **Bwana mwema utusikie.**
Muhudumu Mashamba yazae matunda tele; mavuno yawe mengi.
Wote **Bwana mwema utusikie.**
Muhudumu Mafundi na wafanya biashara wote waone faida kwa kazi zao.
Wote **Bwana mwema utusikie.**
Muhudumu Sisi na adui zetu tuwe na moyo wa kuvunjika na tutafute salama.
Wote **Bwana mwema utusikie.**
Muhudumu Nguvu ya Bwana itegemeze wagonjwa wote.
Wote **Bwana mwema utusikie.**
Muhudumu Mapendo ya Bwana yafariji waliokufiliwa, wanaoteswa, wajane, yatima, na wenye kusikia upekee.
Wote **Bwana mwema utusikie.**
Muhudumu Njia za dunia zisafishwe kwa hatari zo zote.
Wote **Aleluya. Bwana wa rehema ni pamoja nasi. Amina.**

Muhudumu anaweza kualika watu wengine kuomba na maneno haya: Tuendelee kuomba, kwa sisi wenyewe na ndugu na dada zetu...

Kuchunga kimya: wengine wanaweza kuomba kwa sauti, moja kwa moja, na wengine kwa siri. Nyuma ya dakika chache muhudumu aseme:

Tumaini letu ni kwako, Bwana wa rehema.
Wote **Tunategemea wewe pekee,**
Bwana wa mapendo. Amina.

Ona sasa Sala ya Bwana, kwa ukurasa 55, N° 20

- - - - - - - - - - - - *AU* - - - - - - - - - - - -

19b *Muhudumu* Tuombee mahitaji ya Kanisa na dunia.
Baba, tuko watoto wako, ndugu na dada za Mwana wako Yesu Kristo, utusikie, kwani Roho yako inasema ndani yetu tunapoomba.
Wote **Bwana, utusikie.**
Muhudumu Baba, uliumba mbingu na dunia, ubariki mavuno ya mashamba yetu, na kazi za mikono yetu; utupatie hekima na akili kutunza vema inchi yetu na mali yake.
Wote **Bwana, utusikie.**
Muhudumu Baba, ulituumba kwa mufano wako: utufundishe kuheshimu mufano ule katika watu wote.
Wote **Bwana, utusikie.**
Muhudumu Baba, ulituma Mwana wako duniani: akiishi ndani yetu, afunuliwe kwa watu wengine.
Wote **Bwana, utusikie.**
Muhudumu Yesu Kristo, ulituma mitume kwa mataifa yote: ubariki waaskofu wote, na hasa Askofu Mukuu wetu J, pamoja na Askofu wetu J, na watumishi wote wa Kanisa.
Wote **Kristo, utusikie.**
Muhudumu Yesu, uliombea Kanisa, liwe moja: uunganishe wakristo wote, ili dunia iamini.
Wote **Kristo, utusikie.**
Muhudumu Yesu, uliacha utajiri kwa ajili yetu: tia moyo kwa wenye mali kusaidia masikini.
Wote **Kristo, utusikie.**
Muhudumu Yesu, uliponyesha wagonjwa na mukono wako na maneno yako: uponyeshe vile wagonjwa wa siku hizi, na bariki wanaowatunza.
Wote **Kristo, utusikie.**
Muhudumu Yesu, ulishitakiwa uwongo, ukateswa: saidia ndugu na dada zetu wanaoteswa pasipo kosa.
Wote **Kristo, utusikie.**
Muhudumu Mungu, Roho yako aliwezesha manabii ya zamani: asaidie kanisa lako liwe aminifu katika kutangaza kweli duniani.
Wote **Mungu, utusaidie na Roho yako.**
Muhudumu Mungu, Roho yako aliamusha wanafunzi toka huzuni na shaka, watangaze Yesu duniani: kuja kutuamusha, tupashe Habari Njema kwao walio karibu na walio mbali.
Wote **Mungu, utusaidie na Roho yako.**
Muhudumu Mungu, Roho yako, alifunulia maneno ya Biblia kwa waandishi wachaguliwa: utupe akili kuyafahamu, na hodari kuyatii.
Wote **Mungu, utusaidie na Roho yako.**
Muhudumu Mungu wa uwezo, Baba, Mwana, na Roho: sifa iwe kwako, duniani na mbinguni, leo na milele.
Wote **Amina.**
Ona sasa Sala ya Bwana, kwa ukurasa 55, N° 20

- - - - - - - - - - - - *AU* - - - - - - - - - - - -

19c *Muhudumu aseme:*
Tuombee Kanisa na dunia na tumushukuru Mungu kwa wema wake wote.

1. Mungu Mwenyezi, Baba yetu ya mbinguni, kwa Mwana wako Yesu Kristo, umetuahidi kutusikia tukiomba kwa imani:

Tunakushukuru Baba kwa...
Tunaombea...
Kanisa duniani...
Jimbo letu, Dayosisi yetu, na Askofu wetu J...
Ee Mungu, ulipe Kanisa lako nguvu kuendelesha mbele kazi ya Kristo; ili sisi na wote wanaokiri jina lako, tushirikiane katika kweli yako, tuishi pamoja katika mapendo yako, na tuonyeshe utukufu wako duniani.
Ee Bwana kwa rehema yako.
Wote **Usikie kuomba kwetu**
2. Mungu, tunakushukuru kwa...
Tunaombea...
Mataifa yote duniani...
Mutawala wetu na Wakubwa...
Taifa letu...
Watu wote kwa kazi zao za kila siku...
Ee Mungu uwape akili Wakubwa wote wanaotutawala, zaidi Prezidenti yetu J. Tunakusihi uendeleshe taifa letu na mataifa yote kwa njia ya haki na salama; ili watu wote waheshimu mumoja kwa mwingine, na wafuate siku zote uzuri kwa watu wote.
Ee Bwana kwa rehema yako.
Wote **Usikie kuomba kwetu**
3. Mungu, tunakushukuru kwa...
Tunaombea...
Parokia yetu...
Nyumba zetu na rafiki zetu...
Wenye mahitaji yo yote...
Ee Mungu utupe sisi neema, kwa nyumba zetu na kwa
rafiki zetu, na vile kwa jirani zetu zote; sisi sote tukutumikie kwa kuwatumikia, tuwapende kama Kristo anavyotupenda.
Ee Bwana kwa rehema yako.
Wote **Usikie kuomba kwetu**
4. Tunaombea wagonjwa na wanaoumwa na wanaokufiliwa, na wengine wenye magumu, na wale wasioamini Kristo...
Tumushukuru Mungu kwa wale wote wanaowasaidia...
Ee Mungu tunakusihi uwafariji na uwaponyeshe, wale wote walio na mateso ya mwili na ya akili na ya roho. Uwategemeze na uhodari na taraja katika mateso yao; na uwaletee furaha kwa wokovu wako. Na vile tunakushukuru na tunawaombea wale wanaowasaidia na wanaowatunza katika huzuni na mashaka yao.
Ee Bwana kwa rehema yako.
Wote **Usikie kuomba kwetu**
5. Na tunalisifu jina lako takatifu kwa watumishi wako wote wanaotoka katika uzima huu, wanaokuamini na wanaokuogopa. Tunakusihi utupe neema tufuate desturi zao nzuri, tukutane nao katika ufalme wako wa mbinguni. Utupe sisi hivi, Ee Bwana, kama tunavyoviomba kwa Yesu Kristo Mwana wako, Mwokozi wetu. **Amina**.

Ombi hili linaweza kusemwa kama ombi moja pasipo kugawanika.

— — — — — — — — — — — — — — — — — —

20 *SALA YA BWANA. Muhudumu aseme:*
Tuombe, kama Mwokozi wetu alivyotuagiza na namna alivyotufundisha, tusubutu kusema:
Wote **Baba yetu, uliye mbinguni,**
jina lako litukuzwe,
ufalme wako uje,
mapenzi yako yatimizwe,
duniani kama mbinguni.
Utupe leo chakula chetu cha kila siku;

utusamehe makosa yetu,
kama tunavyowasamehe waliotukosea.
Usitulete katika majaribu,
lakini utuokoe katika uovu.
Kwani kwako ufalme,
uwezo na utukufu,
milele na milele, Amina.

SALAMA YA BWANA

21† *Wote wasimame. Mbele ya kuwatakia salama, Kasisi aseme moja kati ya matangulizi haya (kufuatana na wakati wa mwaka au neno kubwa la mahubiri):*

a Sisi ni mwili wa Kristo, kwa sababu katika Roho moja sisi sote tulibatizwa katika mwili mumoja. Ndipo tufuate vinavyotuletea salama, na vinavyojenga maisha yetu, pamoja na wote kila siku. *1 Wakorinto 12:13, Waroma 14:19*

b Kristo Mwokozi wetu ni Mukubwa wa Salama: kuongezwa kwa utawala wake na salama hakutakuwa na mwisho. *Isaya 9:6-7*

c Kristo ni salama yetu. Ametupatanisha na Mungu katika mwili mumoja, kwa njia ya musalaba wake. Tunakutana katika jina lake, tukifurahi pamoja katika salama yake. *Waefeso 2:16*

d Yesu alisema: Ninawaachia salama; ninawapa salama yangu; nami ninawapa ninyi si kama dunia inavyowapa. Musifazaike mioyoni mwenu; wala musiwe na woga. *Yoane 14:27*

e Matunda ya Roho ni mapendo, furaha, salama, uvumilivu, neema, wema, uaminifu, upole, na kujizuiza. Kwa vile tunavyoishi kwa Roho, basi tutafute maongozi ya Roho. *Wagalatia 5:22-23,25*

Kasisi Salama ya Bwana iwe nanyi siku zote
Wote **Iwe pia nawe.**
Kasisi anaweza kusema: Katika mapendo ya Kristo,
tupeane salama
Watu wasalamiane.

SHEREHE YA MEZA YA BWANA

22 *Kasisi atayarishe mukate na mvinyo kwa Meza Takatifu, watu wakiimba wimbo, na kutoa sadaka. Kasisi aombee sadaka.*

Kasisi aseme OMBI LA KUSHUKURU: 22a au 22b au 22c.

— — — — □ — — — —

22a *Kasisi* Bwana awe nanyi
Wote **Awe pia nawe.**
Kasisi Inueni mioyo yenu.
Wote **Tunaiinua kwa Bwana.**
Kasisi Tumushukuru Bwana Mungu wetu.
Wote **Kutenda hivi ni vizuri na vema.**
Kasisi Ndiyo bora kwetu, inatupasa, ni furaha yetu, kila wakati na ndani ya kila pahali, kukushukuru Ee Bwana, Baba Mutakatifu, Mungu Mwenyezi wa milele, kwa Yesu Kristo, Mwana wako wa pekee, Bwana wetu.

Kwani yeye ni Neno lako la uzima, kwa yeye vitu vyote viliumbwa toka mwanzo, nasi tumeumbwa kwa mufano wako. Kwa yeye ulituokoa toka utumwa wa zambi; ukimupa kuzaliwa mutu, kufa musalabani na kufufuka kwa sisi.

Kwa yeye umetufanya kuwa watu wako pekee, ukimutukuza juu kwa mukono wako wa kuume wa utukufu; na kwa yeye umetutumia sisi Roho yako Mutakatifu ya uzima.

Kushukuru kwa nyakati fulani:

_____

KUJA Na sasa tunakushukuru, kwa sababu kwa kuja kwake kama mutu, siku ya kukombolewa kwetu imekaribia; na kwa yeye utafanya yote kuwa mapya, akikuja katika uwezo na ushindi kuhukumu dunia.

KUZALIWA Na sasa tunakushukuru, kwa sababu kwa uwezo wa Roho Mutakatifu, Kristo alitwaa asili yetu na alizaliwa na Bikira Maria mama yake, ili aweze kutu-safisha kwa zambi zetu, na kutufanya wana wako.

ONYESHO Na sasa tunakushukuru, kwa sababu umefunua siri yako ya wokovu, na umemwonyesha Yesu kuwa nuru ya mataifa yote.

KUFUNGA Na sasa tunakushukuru, kwa sababu kwa yeye umetupa sisi Roho ya kutii, ili tuweze kushinda uovu, na kukomea katika neema.

JUMA TAKATIFU Na sasa tunakushukuru, kwa sababu kwa ajili ya wokovu wetu Yesu alitii hata kufa kwa musalaba. Muti wa haya ukageuka muti wa utukufu, na pahali uzima ulipopotea, ni hapo uzima ulirudishwa.

SIKU YA INE YA JUMA TAKATIFU Na sasa tunakushukuru, kwa sababu kwa siku mbele ya kuteswa kwake akiketi pahali pa chakula pamoja na wanafunzi wake, aliamuru siri hizi takatifu; na akiomba usiku ule, alikusudi kutii mapenzi yako hadi musalaba.

SIKU YA KUFUFUKA Na sasa tunakushukuru, kwa sababu alifufuka na utukufu toka wafu. Kwa kufa kwake aliangamiza kufa, na kwa kufufuka kwake ameturudishia uzima wa milele.

KUPANDA Na sasa tunakushukuru, kwa sababu kwa mwili wake wa kufufuka alionekana kwa wanafunzi wake, na mbele ya macho yao akachukuliwa mbinguni, kutawala na wewe katika utukufu.

PENTEKOTE Na sasa tunakushukuru, kwa sababu kwa Roho yule Mutakatifu unatuongoza kwa kweli yote, na unatupa sisi uwezo kutangaza Habari Njema kwa mataifa na kukutumikia kwa ukuhani wa kifalme.

SIKU YA UTATU Na sasa tunakushukuru, kwa sababu umefunua utukufu wako kama utukufu wa Mwana wako na wa Roho Mutakatifu, nafsi tatu walio sawa katika enzi, wasiogawanyika katika utukufu, lakini Bwana mumoja, Mungu mumoja anayeabudiwa na kutukuzwa milele.

WATAKATIFU Na sasa tunakushukuru, kwa tumaini la mwito wetu ulilotupa sisi katika watakatifu wako; ili tukifuata mufano wao na kupata nguvu kwa ushirika wao, tupige mbio na uvumilivu katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu, na pamoja nao tupokee taji isiyoharibika.

Kasisi Kwa hivyo sisi pamoja na malaika na malaika wakuu, na kundi lote la mbinguni, tunakutukuza na kulisifu jina lako takatifu. Tunakusifu daima, tukisema:

Wote **Mutakatifu, Mutakatifu, Mutakatifu,**
Bwana Mungu wa uwezo na mamlaka,
mbingu na inchi zimejaa utukufu wako,
utukufu uwe nawe, Ee Bwana uliye mbinguni.
Abarikiwe anayekuja kwa Jina la Bwana.
Hosana juu mbinguni.

Kasisi Ee Baba ya mbinguni, upokee kusifu kwetu katika Mwana wako, Mwokozi wetu Yesu Kristo, na tukipokea mukate huu na kikombe hiki kama Mwana wako alivyotuamuru, tuwe washiriki wa mwili na damu yake.

Usiku ule alipotolewa alitwaa mukate[a] na alipokwisha kukushukuru, akauvunja[b] akawapa wanafunzi wake akisema:

«Twaeni, mule,[c] huu ni Mwili wangu
unaotolewa kwa ajili yenu;
fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi.»

Ndivyo, walipokwisha kula,[d] akatwaa kikombe; alipokwisha kukushukuru, akawapa, akisema:

«Ninyi wote munywe hii,
kwani hii ndiyo[e] Damu yangu ya Agano Jipya,

inayomwangika kwa ajili yenu, na kwa watu wengi,
kwa kusamehewa kwa zambi;
fanyeni hivi, kila mara munapoikunywa
kwa kunikumbuka mimi.»

Wote **Kristo alikufa;**
Kristo amefufuka;
Kristo atakuja tena.

Kasisi Ndiyo Baba ya mbinguni, kwa mukate huu na kikombe hiki tunafanya hivi kumukumbuka. Tunaonyesha na kutangaza zabihu yake kamilifu musalabani mara moja; tunatangaza ufufuko wake toka wafu, na kupanda kwake mbinguni, na tunangojea kuja kwake katika utukufu.

Katika yeye, kuhani yetu mukubwa, upokee zabihu yetu ya kusifu na kushukuru, na kwa kula na kunywa zawadi hizi takatifu, mbele ya utukufu wako, tuwe wapya kwa Roho yako; utuingize mapendo yako, na utuunge pamoja katika mwili wa Mwana wako.

Naye, na katika yeye, na kwa uwezo wa Roho Mutakatifu, pamoja na wote wenye kusimama mbele yako, kwa inchi na mbingu, tunakuabudu, Baba Mwenyezi, sasa hata milele:

Wote **Baraka na heshima, na utukufu na uwezo,**
uwe kwako milele na milele. Amina.

Ona sasa N° 23, ukurasa 64

AU -

22b *Kasisi aseme*: Bwana awe nanyi

Wote **Awe pia nawe.**

Kasisi Inueni mioyo yenu.

Wote **Tunaiinua kwa Bwana.**

Kasisi Tumushukuru Bwana Mungu wetu.

Wote **Kutenda hivi ni vizuri na vema.**

Kasisi Ndiyo, ni furaha yetu kukushukuru,
Ee Baba ya mbinguni, kwani uliumba vitu vyote:
nyota, jua, mwezi, na dunia hii;
milima na bonde, pori na shamba,
mito na bahari,
na wenyeji wao wote.
Ukaumba watu,
ukiwapa akili na uwezo kupita wanyama wote;
ukachagua taifa moja kukujua zaidi.
Tunakushukuru,
kwani wakati watu walizarau mapenzi yako,
uliwaita kurudi katika njia zako,
ukijaza manabii na Roho yako Mutakatifu,
ili wawe washuhuda wa uwezo na haki yako.
Namna nabii Isaya alivyosikia hekaluni,
sisi pamoja na malaika na malaika wakuu,
na kundi lote la mbinguni, tunakusifu daima, tukisema,

Wote **Mutakatifu, Mutakatifu, Mutakatifu,**
Bwana Mungu wa uwezo na mamlaka,
Mbingu na inchi zimejaa utukufu wako,
Utukufu uwe nawe, Ee Bwana uliye mbinguni.
Abarikiwe anayekuja kwa Jina la Bwana.
Hosana juu mbinguni.

Kasisi Tunakushukuru, Ee Baba ya mapendo,
kwani ulituma Mwana wako,
kuzaliwa kama mutu,
kutuonyeshea mufano wako,

na kuokoa watu wa mataifa yote,
akikufa kwa ajili yetu musalabani.
Usiku ule alipotolewa alitwaa mukate, (a)
na alipokwisha kukushukuru, akauvunja (b)
akawapa wanafunzi wake akisema:
«Twaeni, mule, (c) huu ni Mwili wangu
unaotolewa kwa ajili yenu;
fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi.»
Ndivyo, walipokwisha kula, (d) akatwaa kikombe;
alipokwisha kukushukuru, akawapa, akisema:
«Ninyi wote munywe hii,
kwani hii ndiyo(e) Damu yangu ya Agano Jipya,
inayomwangika kwa ajili yenu,
na kwa watu wengi,
kwa kusamehewa kwa zambi;
fanyeni hivi, kila mara munapoikunywa
kwa kunikumbuka mimi.»
Wote **Kristo alikufa;**
Kristo amefufuka;
Kristo atakuja tena.
Kasisi Tunakushukuru kwani ulitimiza ahadi ya Yesu,
ukitutumia Musaidizi, Roho Mutakatifu,
ili Habari Njema ya mapendo yako
ijulikane po pote duniani.
Na sasa, tukifanya hii kumukumbuka Yesu,
ukubali, katika uwezo wa yule Roho,
tuwe washiriki wa mwili na damu yake.
Utufanye wapya katika Roho yako,
ili sisi pamoja na kanisa lako po pote,
tutumikie jirani zetu katika mapendo yako,
tuvute watu wote kwako,
na tuonyeshe utukufu wako,
Baba Mwenyezi, sasa hata milele:
Wote **Baraka na heshima,**
na utukufu na uwezo,
uwe kwako milele na milele. Amina.

Ona sasa N° 23, ukurasa 64

- - - - - - - - - - - - *AU*- - - - - - - - - - -

22c *Kasisi* Baba Mwenyezi,
uliye nasi saa zote na pahali pote,
tunainua mioyo na sauti zetu kutukuza jina lako:
Wote **Tunasifu jina lako takatifu!**
Kasisi Mungu ndiwe Mutakatifu, mukamilifu,
kisima cha haki na kweli:
wewe ni nuru, hakuna giza ndani yako,
na unachukia zambi zote.
Wote **Tunasifu jina lako takatifu!**
Kasisi Ndiwe mwenye mapendo
hata kwa sisi wenye zambi:
unataka kukusanya watoto wako wapotevu
chini ya mabawa yako;
kila mara unatuita kurudi kwako.
Wote **Tunasifu jina lako takatifu!**
Kasisi Ulituma Mwana wako,

kuzaliwa na Bikira Maria,
awe mutu sawa nasi, lakini pasipo zambi,
ukamujaza na Roho yako Mutakatifu.

Wote **Tunashukuru Yesu Kristo, alikuja kutuokoa!**

Kasisi Alijinyenyekeza kuwa mutumishi wa wote:
akaponyesha, akafundisha,
akakaribia waliokataliwa na wengine.
Kwa ajili ya wokovu wetu, alikufa musalabani,
akafufuka toka wafu, akapanda mbinguni.

Wote **Tunashukuru Yesu Kristo, alikuja kutuokoa!**

Kasisi Mbele ya kifo chake, mezani na wanafunzi wake:
alitwaa mukate,[a] akakushukuru, akauvunja,[b]
akawapa, akisema:
«Twaeni mule,[c] huu ni Mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu.»
Halafu akatwaa kikombe [d], akakushukuru,
akawapa, akisema:
«Hii ndiyo Damu yangu ya Agano Jipya,[e]
inayomwangika kwa ajili yenu,
na kwa watu wengi,
kwa usamehe wa zambi.
Fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi.»

Wote **Tunashukuru Yesu Kristo, alikuja kutuokoa!**

Kasisi Hakuacha rafiki zake yatima,
kwani Roho yako Mutakatifu alikuja kuwafariji, kuwatakasa, na kuwawezesha.
Baba, tunakushukuru daima,
kwani Roho yule analeta uzima, umoja na uwezo.

Wote **Roho yako Mutakatifu awe nasi kila siku!**

Kasisi Leo tukikumbuka Kristo hivi,
katika uwezo wa Roho yako
mukate huu uwe kwa sisi mwili wake,
na mvinyo hii iwe kwa sisi damu yake,
ili mioyo yetu isafishwe,
na tuwe tayari kutii mapenzi yako.

Wote **Roho yako Mutakatifu awe nasi kila siku!**

Kasisi Uamushe kanisa lako,
liwe chumvi, chachu na nuru duniani,
likishuhudia utakatifu na mapendo yako,
tukingoja kurudi kwake Kristo katika utukufu.

Wote **Roho yako Mutakatifu awe nasi kila siku!**

Kasisi Tutakuabudu Mungu Mutakatifu,
pasipo kuacha, duniani na mbinguni,
milele na milele.

Wote **Aleluya, aleluya, aleluya! Amina.**

— — — — — — — — — — — — — — — — — —

23 *Kasisi* Tujitayarishe kupokea Chakula cha Bwana:

Wote **Hatusubutu kuikaribia Meza yako hii,**
Bwana mwenye rehema,
kwa kuitumainia haki yetu wenyewe,
ila rehema zako nyingi zilizo kubwa.
Hatustahili hata kuokota makombo chini ya Meza yako.
Ndiwe Bwana usiyegeuka,
asili yako ni kuwa na rehema daima.
Basi utupe, Bwana mwema,
tuule mwili wa Mwana wako mupendwa Yesu Kristo,

na kuinywa damu yake,
tukae daima ndani yake,
naye ndani yetu. Amina.

24 *Kasisi aseme:*
Mukaribie na imani, mupokee sakramento hii takatifu ya mwili na damu ya Kristo tukikumbuka alikufa kwa ajili yetu na tumule mioyoni mwetu kwa imani tukishukuru.

Kisha Kasisi na Wahudumu wengine wapokee mukate na mvinyo.

25* *Halafu mwenye kugawa mukate aseme:*
Mwili wa Bwana wetu Yesu Kristo, uliotolewa kwa ajili yako, ukulinde mwili na nafsi hata uzima wa milele. Twaa huu; ule ukikumbuka Kristo alikufa kwa ajili yako, nawe umule moyoni mwako na imani na kushukuru.

Na mwenye kugawa mvinyo aseme:
Damu ya Bwana wetu Yesu Kristo iliyomwangika kwa ajili yako, ikulinde mwili na nafsi hata uzima wa milele. Unywe hii ukikumbuka Damu ya Kristo ilimwangika kwa ajili yako, na ushukuru.

26 *Halafu wahudumu wagawe mukate na mvinyo kwa watu, wakitumia maneno ya 26a, 26b au 26c. Wakati watu wanapokea, kwanza iwe kimya, lakini nyuma kidogo nyimbo za hali ya maombi zinaweza kuimbwa.*

— — — — □ — — — —

26a *Mwenye kugawa mukate au mvinyo, aseme kwa kila mutu:*
Mwili wa Kristo. *au* Damu ya Kristo.
Na kila mumoja mwenye kupokea ajibu: Amina.

- - - - - - - - - - - - *AU* - - - - - - - - - - - -

26b *Kwa mukate:*
Twaa huu, ule ukikumbuka Kristo alikufa kwa ajili yako na kushukuru.
Na kwa kikombe:
Unywe hii, ukikumbuka Damu ya Kristo iliyomwangika kwa ajili yako, na kushukuru.

- - - - - - - - - - - - *AU* - - - - - - - - - - - -

26c *Kwa mukate:* Mwili wa Kristo, mukate wa mbinguni.

Kwa mvinyo: Damu ya Kristo, kikombe cha wokovu.
Na kila mumoja mwenye kupokea ajibu: Amina.

— — — — — — — — — □ — — — — — — — — —

27* *Kama mukate na/au mvinyo zilizotakaswa zimemalizika na watu wote hawajashiriki bado, Kasisi aongeze nyingine akisema maneno haya, na akiweka mikono yake juu ya ongezo lile.*
Baba wa rehema, tukikumbuka Mwana wako, aliyetoa mwili wake na damu yake kwa ajili yetu, ukubali vile...
...tukikula mukate huu tuwe washiriki wa mwili wake;
...(na) tukikunywa mvinyo hii tuwe washiriki wa damu yake;
katika uwezo wa Roho Mutakatifu. Amina.

28 *Kama mukate na mvinyo zilizotakaswa zinabaki, zimalizikwe na kasisi na washiriki wengine atakaowaita, mara moja au baada ya Baraka, kwa heshima.*

KUTOKA KWA WATU WA MUNGU

29 *Wote waseme moja la maombi haya:*

— — — — □ — — — —

29a **Mungu Mwenyezi,**
tunakushukuru kwa kutulisha
na mwili na damu ya Mwana wako, Yesu Kristo.
Kwa yeye tunakutolea mioyo na miili yetu
kuwa zabihu iliyo hai.
Ututume duniani
kwa uwezo wa Roho yako,
kuishi na kutumika,
kwa sifa na utukufu wako. Amina

- - - - - - - - - - - - *AU* - - - - - - - - - - - -

29b **Baba ya wote,**
tunakusifu, tunakushukuru,
kwani wakati tulikuwa wapotevu
ulitutumia Mwana wako
kuturudisha nyumbani mwako.
Kwa maisha yake na musalaba wake
alitangaza mapendo yako
akatupatia neema
akafungua mulango wa utukufu.
Sisi tuliopokea mwili wake:
tuishi katika ufufuko wake;
sisi tuliokunywa kikombe chake:
tutangaze wokovu kwa wengine;
sisi tunaoangaziwa na Roho yako:
tuwe nuru katika dunia.
Utuchunge imara kwa tumaini la wokovu,
ili sisi na watoto wako wote tuwe huru,
na dunia nzima iishi kusifu jina lako,
kwa Yesu Kristo Bwana wetu. Amina.

— — — — — — — — — — □ — — — — — — — — —

30* *Shairi la kila wakati lisomwe.*

31† *Kasisi au Askofu akiwapo, aseme Salama na Baraka,au Baraka ya kila wakati.*

— — — — □ — — — —

Salama ya Mungu, inayopita akili yote,
iwalinde mioyo na nia zenu,
katika hali ya kujua na kupenda Mungu,
na Mwana wake, Yesu Kristo Bwana wetu;
na baraka ya Mungu Mwenyezi,
Baba na Mwana, na Roho Mutakatifu,
iwe kwenu na ikae nanyi,
milele na milele. **Amina.**

- - - - - - - - - - - - *AU* - - - - - - - - - - - -

KUJA Kristo, Jua la haki, awaangazie, na aondoe giza njiani mwenu; na baraka...

KUZALIWA Kristo Mwana wa Mungu afurahishe mioyo yenu na Habari Njema za Ufalme wake; na baraka...

KUFUNGA Kristo awape neema kukomea katika utakatifu, kukataa tamaa za dunia, kuchukua musalaba, na kumufuata; na baraka...

JUMA TAKATIFU Kristo aliyesulibiwa awavute kwake, ili mupate musingi kweli wa imani, tegemeo imara kwa tumaini, na hakika ya usamehe wa zambi; na baraka...

KUFUFUKA Mungu wa salama, aliyeleta toka wafu Bwana wetu aliye Muchungaji mukuu wa kondoo, awafanye ninyi kuwa wakamilifu katika kila kazi njema,

mupate kufanya mapenzi yake, naye afanye ndani yenu neno linalomupendeza, na baraka...

KUPANDA Kristo Mufalme wetu awafanye waaminifu na wavumilivu kutenda mapenzi yake, ili mutawale pamoja naye katika utukufu na baraka...

PENTEKOTE Mungu aamushe zawadi ya Roho Mutakatifu iliyo ndani yenu, ili mukiri kwamba Yesu Kristo ni Bwana, na kutangaza furaha ya Habari Njema ya milele pahali po pote na baraka...

UTATU Mungu Utatu Mutakatifu aongeze nguvu yenu kuamini na kupenda; awalinde kwa pande zote; na awaongoze katika kweli na salama na baraka...

WATAKATIFU Mungu awape neema kufuata watakatifu wake katika imani, na tumaini na mapendo na baraka...

...na baraka ya Mungu Mwenyezi,
Baba na Mwana, na Roho Mutakatifu,
iwe kwenu na ikae nanyi, milele na milele. **Amina.**

— — — — — — — — — □ — — — — — — — — —

32 *Muhudumu aondoe watu na maneno haya:*

— — — — □ — — — —

Wakati wa UFUFUKO:

Muhudumu Bwana wetu akae nanyi,
Wote **Akae na roho yako.**
Muhudumu Kwendeni na salama kwa kumupenda na kumutumikia Bwana. Aleluya!
Wote **Kwa Jina la Kristo. Aleluya! Amina.**

- - - - - - - - - - - - *AU* - - - - - - - - - - - -

NYAKATI NYINGINE:

Muhudumu Bwana wetu akae nanyi,
Wote **Akae na roho yako.**
Muhudumu Kwendeni na salama kwa kumupenda na kumutumikia Bwana.
Wote **Kwa Jina la Kristo. Amina.**

— — — — — — — — — □ — — — — — — — — —

32* *Wimbo wa kumaliza ibada.*